JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Sheikhbad,
S.L.P. 1004,
65101LINDI,
Barua Pepe: rbclindi@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

LINDI , 27 JANUARI, 2021

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU MKOA WA LINDI YAOKOA SH 91,731,513.00 ZIKIWA NI MAPUNJO YA MALIPO YA WAKULIMA WA KOROSHO, UFUTA NA FEDHA ZA SERIKALI.

Ndugu WanaHabari,

TAKUKURU (M) LINDI inajumuisha ofisi ya TAKUKURU Mkoa pamoja na ofisi za Wilaya Nne (4) ambazo ni Kilwa, Nachingwea, Liwale na Ruangwa. Katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2020/2021 ilioanzia Oktoba, 2020 hadi Desemba, 2020, Ofisi za TAKUKURU katika Mkoa wa Lindi zimefanya kazi na kutekeleza majukumu mbalimbali kwa namna yanavyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 iliyorejewa mwaka 2019. Majukumu hayo yalifanywa kupitia madawati mbalimbali ikiwemo dawati la Uchunguzi, Huduma za Sheria na Mashitaka, Utafiti na Udhibiti pamoja na Elimu kwa Umma.

Ndugu WanaHabari,

Kupitia dawati la uchunguzi, kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Lindi ilipokea jumla ya malalamiko 86 yanayohusiana na vitendo vya rushwa na mambo mengine yanayoshabihiana na vitendo hivyo.

Malalamiko haya yalihusu sekta mbalimbali zikiwemo: Elimu (4), Ardhi (8), Kilimo (3), Ushirika (28), Afya (6), Fedha (6), Jeshi la Polisi (1), Mahakama (6), Nishati (7), Siasa (5),

Binafsi (9), Uvuvi na Misitu (3). Malalamiko haya yamefanyiwa kazi na yapo katika hatua mbalimbali mbalimbali na baadhi yamekamilika.

Ndugu waandishi wa habari,

Katika kipindi hiki, TAKUKURU Mkoa wa Lindi imefanikiwa kudhibiti na kuokoa fedha jumla **shs 91,731,513.00.** Fedha hizo zilizookolewa zinajumuisha fedha za wakulima kwa mauzo ya ufuta katika msimu wa mwaka 2019/2020, fedha za mauzo ya korosho katika msimu wa mwaka wa mwaka 2020/2021, pamoja na Miradi mbalimbali ya maendeleo na kodi ya mapato ya serikali. Kati ya fedha hizo zilizookolewa, Jumla ya sh. **22,836,168.00** zilirejeshwa serikalini kupitia akaunti ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU na **shs 68,895,345.00** zimeokolewa na kurejeshwa kwa wakulima ambao walikuwa wamedhurumiwa fedha hizo.

Ndugu WanaHabari,

Kwa upande wa mashitaka, katika kipindi cha mwezi Oktoba - Desemba, 2020 TAKUKURU (M) Lindi ilifanikiwa kukamilisha kesi mbili 2 mahakamani ambapo kesi moja 1 kati ya hizo Mshitakiwa alipatikana na hatia na amehukumiwa na nyingine moja Mshitakiwa aliachiwa huru.

Ndugu WanaHabari,

Katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Lindi kupitia Dawati la Kuzuia Rushwa ilifuatilia matumizi ya fedha za mradi mmoja wa maendeleo (Mradi wa Maji kijiji cha NAMIKONGO – NACHINGWEA) wenye thamani ya sh **315,374,112.00.** mradi huu umekamilika na umeanza kutumika.

Ndugu WanaHabari,

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendelea kutekeleza malengo yake ya dawati la elimu kwa umma kwa kuwaelimisha wananchi wa makundi mbalimbali na wadau wengine ikiwa ni mtu mmoja mmoja, jamii, taasisi na taifa kwa ujumla juu ya rushwa na madhara yake.

Katika kipindi hiki TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendesha semina 40, imefanya mikutano ya hadhara 14. Pia TAKUKURU (M) Lindi imefanya ufunguzi na uimarishaji wa klabu za wanafunzi za wapinga rushwa 108, vipindi vya TV na Redio 04 na Utoaji wa makala au uandishi wa habari 08.

Ndugu WanaHabari,

Katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 iliyoanza Januari, 2021 TAKUKURU Mkoa Lindi imejipanga kuongeza juhudi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliopo Mkoani Lindi ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na miradi ya ujenzi wa miundombinu wa madarasa ya shule za Msimgi pamoja na shule za Sekondari. kukamilisha kuchambua mifumo ya ukusanyaji wa kodi na mapato ya serikali na kisha kuendesha warsha na wadau mbalimbali, na kuendelea kuelimisha umma madhara yaletwayo na vitendo vya rushwa.

Jambo la mwisho ambalo ningependa umma wa Wananchi wa Lindi ufahamu ni kwamba **kuanzia Januari Mwaka 2021** tumeanzisha utaratibu wa **MOBILE PCCB – TAKUKURU INAYOTEMBEA,** kwa kutenga **siku moja kila mwezi** ambapo kila ofisi ya TAKUKURU mkoa na wilaya itawafuata wananchi huko walipo kwa lengo la kusikiliza pamoja na kutatua kero zao. Kwa mkoa wa Lindi mwezi huu tutasikiliza kero tarehe kesho 28 kata ya Rasibura eneo la Mitwerona kwa mwezi ujao tutawajulisha ni tarehe ngapi na tutakuwa wapi.

TAKUKURU mkoa wa Lindi inaendelea kuwashukuru wananchi wa mkoa wa Lindi na kuzishukuru taasisi mbalimbali (binafsi na za serikali) Mkoani Lindi kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa ofisi yetu za TAKUKURU. Aidha, tunawaomba wananchi na wadau wote waendelee kutuunga mkono kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali hususani kupitia simu yetu ya bure ya **113** kwani mapambano dhidi ya rushwa sio ya TAKUKURU peke yake bali ni ya jamii nzima kwa ujumla.

Imetolewa na:

MHA. ABNERY J. MGANGA

MKUU WA TAKUKURU (M) LINDI